# Kamati ya Bunge yaipongeza serikali uwekezaji Nguru Hills

**Na Mwandishi Wetu, Morogoro**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imeipongeza serikali kwa uwekezaji katika machinjio ya Nguru Hills Mvomero mkoani Morogoro.

Kamati hiyo ikashauri kuhakikisha nyama inayozalishwa katika kiwanda hicho inakubalika kimataifa ili kupata soko la uhakika hasa kwa soko la nje ya nchi.

Wajumbe wa kamati hiyo walisema hayo walipotembelea machinjio ya kisasa yaliyopo Mvomero mkoani Morogoro.

Mradi wa machinjio hayo unaendeshwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kwa kushirikiana na wabia wenza ambao ni kampuni ya Eclipse Investment LLC na kampuni ya Busara Investment LLP.

"Hongereni, tumeona kazi hii nzuri, uwekezaji ni mzuri sana. Tunawapongeza na pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake kubwa.

"Tunamwombea nia yake kwa taifa letu ifanikiwe. Uwekezaji huu ni matokeo ya sera nzuri za serikali yetu," alisema Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatma Tawfiq.

Tawfiq aliwataka wajumbe wa kamati hiyo kwa pamoja kuhakikisha wanaishauri serikali na wawekezaji wengine ili kiwanda hicho kithibitishwe kimataifa ili bidhaa zake ziweze kuuzwa katika soko lolote ulimwenguni.

Mjumbe wa kamati hiyo ya bunge, Kabula Shitobelo aliupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kazi nzuri.

Mjumbe mwingine, Sophia Mwakagenda alieleza kuridhishwa na uwekezaji huo ambao tayari umetoa ajira kwa vijana 300 na akashauri kuwepo na usimamizi ili kiwanda kiwe na tija kwa taifa.

"Mradi huu unakwenda kuwa mkombozi mkubwa kwa wafugaji na wajasiriamali kwani wakiutumia vizuri, utawasaidia kuongeza kipato," alisema Mjumbe mwingine, Neema Mwandabila.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba alisema katika kuhakikisha nyama ya nguru inawafikia Watanzania wengi wa kiwanda wana mpango wa kufungua maduka maeneo mengi ya nchi na kwa kuanzia, tayari kuna duka lililofunguliwa Morogoro mjini.

Mining Officer, Sabai Nyasil. (Photo by Staff Photographer)



MEMBERS of the Parliamentary Social Welfare and Development Committee listen to Nguru Ranch Hills Feedlot management on how they stick to quality of meat served to the public during their tour at PSSSF investment Centre Mvomero District, Morogoro Region, recently. (Photo by Correspondent)

CamScanner

# Wizara yamshukuru Rais Samia ujenzi Bandari Uvuvi Kilwa

**Na Magnus Mahenge**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Sh bilioni 266.7 kugharamia ujenzi wa mradi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko mkoani Lindi.

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa juzi baada ya kurejea kutoka Bandari ya Kilwa Masoko mkoani Lindi, Profesa Shemdoe alisema bandari hiyo ya uvuvi ikikamilika itakuwa msaada mkubwa kwa Watanzania wanaofanya kazi ya uvuvi.

Mradi huo ni miongoni mwa miradi itakayotembelewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo Machi 16, 2023 kwa lengo la kukagua miradi inayotekelezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi mkoani Lindi.

Aidha, Profesa Shemdoe alisema bandari hiyo itatoa ajira 30,000 kwa vijana wa kike na wa kiume, itaongeza usafirishaji wa samaki nje ya nchi na itaongeza tija ya uvuvi Bahari Kuu.

Vilevile, Katibu Mkuu aliainisha faida nyingine kuwa itapunguza upotevu wa samaki, itaondoa changamoto ya uvuvi haramu usioratibiwa na kutolewa taarifa.

Alisema pia itapunguza changamoto ya upungufu wa samaki ndani ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuongeza mchango wa sekta ya uvuvi kutoka asilimia 1.71 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia tatu hadi tano ifikapo 2026.

Profesa Shemdoe alisema tayari Rais Samia ameshaidhia malipo ya awali ya jumla ya Sh bilioni 40 na zimeshalipwa kwa mkandarasi anayejenga bandari hiyo.

Katika ziara hiyo, Katibu Mkuu amekutana na mkandarasi anayejenga bandari hiyo kampuni ya China Harbour Engineering Company Ltd pamoja na Mkandarasi Mshauri Elekezi Dar Al-Handasah Consultants na kuwaelekeza kuwa wafanye kazi kwa bidii ili wamalize ujenzi huo kwa muda uliopangwa.

Kwa upande wake, mkandarasi anayejenga bandari hiyo pamoja na mkandarasi mshauri mwelekezi wamekubali kuwa watafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha kuwa mradi huo unakamilika kwa muda uliopangwa.

Awali, Profesa Shemdoe alisema kuwa anamshukuru Rais Samia kwa kuendelea kumuamini na kumhamishia wizara ya mifugo na uvuvi.

# Wafugaji wahadharishwa kutibu mifugo kiholela

Na Lucy Ngowi

MENEJA wa Kiwanda cha chanjo Tanzania kilichopo chini ya Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Charles Mayenga ameonya tabia ya wafugaji kutibu mifugo kiholela, kwa kuwa inasababisha usugu wa vimelea wa magonjwa dhidi ya dawa.

Mayenga ambaye pia ni daktari wa mifugo, alisema hayo alipozungumza na gazeti hili ofisini kwake.

Alisema katika miaka ya karibuni kuwekuwapo na tatizo la watu kutibu mifugo bila kujua wanachotibu.

"Nasisitiza wafugaji kupima magonjwa ya mifugo kabla ya kuwatibu ili kujua hakika tunakwenda kumtibu yule mgonjwa kwa dawa sahihi. Mchungaji anaamka asubuhi anakuta mifugo yake inaonyesha haina afya, anaingia ndani ana chupa yake ya dawa anavuta na kwenda kumchoma. Hapo hajui anatibu nini," alisema.

Alisema matokeo yake dawa iliyotumika iliyokuwa inatibu ugonjwa mwingine, inakuwa haiwezi kuutibu ugonjwa huo kwa kuwa vijidudu vinakuwa vimezoea.

"Wadudu ni wajanja sana, unapopeleka dawa wao wanaisema hiyo dawa ni ya namna gani halafu wanatengeneza kinga kuhakikisha kuwa haiwadhuru. Baada ya muda wanaizoea na mwisho haiwaui kwa sababu wamejua namna ya kuikwepa," alisema.

"Matokeo yake kwa sababu na sisi tunakula yale mazao ya wanyama, unapokula mnyama ambaye alitibiwa na dawa zile, zinaingia kwako kwa sababu zipo chini ya kiwango," alisema.

Aliongeza: "Wadudu walewale wanaizoea kwenye mwili wako na siku utakapougua ugonjwa kama huo ukienda hospitali na ukipewa dawa ile ambayo au ilikuwa inakutibu kwa sababu wadudu wale wameshaizoea na kujenga usugu dhidi yake hautaweza kutibu."

Alisema wakala inasisitiza wafugaji kutumia maabara zilizopo ili kupata huduma hiyo ya kutambuliwa kwa magonjwa kabla ya kuyatibu ili yatibiwe kwa usahihi waondokane na hilo tatizo.